GAZETI RASMI LA SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

(Hupigwa Chapa kwa Amri ya Serikali)

Sehemu ya CXXXII Nam. 7146 **06 Oktoba, 2023** **Bei Shs.7,000/=**

Imekubaliwa na Mkuu wa Posta kuwa ni Gazeti *Hutolewa kila Ijumaa*

YALIYOMO Ukurasa

Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar Nam.2 ya 2005
Kanuni za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar,
(Fao la kuumia kazini)
[Chini ya kifungu cha 44 (1)]..... 476

SEHEMU YA SHERIA

Tangazo la Sheria liliyotajwa hapo chini yametangazwa katika ***Gazeti Rasmi*** hili.

Tangazo la Sheria

Nam. 109:- Kanuni za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar. (Fao la Kuumia kazini)

Matangazo yaliyohusu maiti, kuvunjikia kwa Ushirika na baadhi ya matangazo ambayo ni muhimu kwa watu kujua yanaweza kutiwa katika Gazeti. Nakala matangazo namna hiyo, zipelekwe kwa Mhariri wa Gazeti Rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar - Tanzania katika nyumba ya kupiga Chapa, Sanduku la Posta 261. Nakla zisichelewe kuliko Jumatatu kila wiki.

SHERIA YA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR, NAM. 2 YA 2005

KANUNI ZA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR (FAO LA KUUMIA KAZINI)

[Chini ya kifungu cha 44(1)]

MPANGILIO WA KANUNI

KANUNI: **MAELEZO:**

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Matumizi.
3. Ufafanuzi.

SEHEMU YA PILI
KUANZISHWA KWA SKIMU YA FIDIA

4. Kuanzishwa kwa Skimu.
5. Chanzo cha fedha za Skimu.
6. Matumizi ya fedha za Skimu.
7. Kazi za Skimu.
8. Wajibu wa Mwajiri katika Skimu.

SEHEMU YA TATU
HAKI YA FAO LA KUUMIA KAZINI NA UKOKOTOAJI WA MAFAO YANAYOLIPWA NA SKIMU

9. Haki ya Fao la Kuumia Kazini.
10. Mafao yanayolipwa na Skimu.
11. Fao la kupatwa na majeraha na ulemavu wa muda.
12. Fao la ulemavu wa Kudumu ambao haumzuii mfanyakazi kurejea kazini.
13. Fao la ulemavu wa kudumu ambao unamzuia mfanyakazi kurejea kazini.
14. Fao la mhudumu wa mfanyakazi mgonjwa ambaye asiyejiweza na asiyeweza kurejea kazini.
15. Fao la kifo kwa wategemezi wa mfanyakazi.
16. Fao la kuumia kazini kwa wanafunzi wanaofanya mafunzo kwa vitendo.

17. Ajali wakati wa kwenda na kurejea kazini.
18. Ajali wakati wa mafunzo au huduma za dharura.
19. Ajali iliyotokea au maradhi yaliyopatikana nje ya Zanzibar.
20. Ajali au maradhi yaliyotokea ndani ya Zanzibar.
21. Fao la kuumia kazini kutokupunguzwa au kunyimwa.
22. Malipo ya mafao kwa mtu ambaye alishawahi kulipwa.
23. Katazo la kukata au kupunguza mshahara.
24. Kuacha au kusamehe fao la kuumia kazini.
25. Vitisho na kulazimisha kunakatazwa.
26. Msaada wa matibabu na mazishi.
27. Nyongeza ya Kiwango cha Mafao.
28. Mfumo wa Malipo.

SEHEMU YA NNE
UTARATIBU WA MAOMBI YA FAO LA KUUMIA KAZINI

29. Taarifa ya ajali.
30. Taarifa ya maradhi yanayotokana na kazi.
31. Taarifa ya kifo cha mfanyakazi.
32. Ombi la fao la kuumia kazini.
33. Kupokelewa kwa ombi la fao.
34. Tathmini ya ajali au maradhi.
35. Kukubaliwa au kukataliwa kwa fomu ya ombi au fomu ya tathmini.
36. Ukokotoaji wa fao la kuumia kazini.
37. Kupitwa na muda kwa ombi la fao.

SEHEMU YA TANO
MASHARTI YA FEDHA

38. Hesabu za Skimu.
39. Bajeti ya Skimu.
40. Ripoti za mwaka za Skimu.

SEHEMU YA SITA
MASHARTI MENGINEYO

41. Makosa na Adhabu.
42. Tathmini ya uhimilivu wa Skimu.
43. Ukaguzi wa sehemu za kazi.
44. Kupata taarifa za Skimu.

JADWELI

TANGAZO NAM. 109

SHERIA YA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR, NAM. 2 YA 2005

KANUNI ZA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR (FAO LA KUUMIA KAZINI)

[Chini ya kifungu cha 44(1)]

KWA UWEZO niliopewa chini ya kifungu cha 44(1) cha Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar Nam. 2 ya 2005, Mimi **DKT. SAADA MKUYA SALUM,** Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha na Mipango natunga Kanuni zifuatazo:

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (Fao la Kuumia Kazini), 2023 na zitaanza kutumika mara baada ya kutiwa saini na Mheshimiwa Waziri na kutangazwa katika Gazeti.

Matumizi.

2.-(1) Kanuni hizi zitatumika Zanzibar kuhusiana na malipo ya fao la kuumia kazini kwa wafanyakazi wote wa sekta ya umma na binafsi ambao ni wanachama wa Mfuko.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, Kanuni hizi zitatumika kwa wafanyakazi wanaofanya kazi Tanzania Bara ambao waajiri wao wanafanya shughuli rasmi za taasisi Zanzibar au Makao Makuu ya taasisi anayofanyia kazi iko Zanzibar.

(3) Malipo ya fao la kuumia kazini yataanza kulipwa kwa wafanyakazi kuanzia tarehe 1 Julai, 2023 kwa ajali, maradhi yanayotokana na kazi au kifo kilichotokea kuanzia tarehe 1 Julai, 2023.

(4) Waziri anaweza, kwa kushauriana na Bodi, kujumuisha wafanyakazi wengine wowote au kundi la wafanyakazi katika Skimu kwa madhumuni ya kulipwa fao la kuumia kazini kwa kutumia masharti ya Kanuni hizi.

Ufafanuzi.

3. Katika Kanuni hizi, isipokuwa maelezo yatahitaji vinginevyo:

"Ajali" maana yake ni tukio lililotokea bila kutarajia au kupanga katika kutekeleza majukumu ya kazi ya mfanyakazi husika ambalo limepelekea majeraha, ulemavu, maradhi au kifo cha

mfanyakazi;

"Ajali kazini" maana yake ni ajali iliyompata mfanyakazi wakati wa kazi, katika sehemu yake ya kazi au katika sehemu nyengine yoyote ambayo mfanyakazi asingekuwepo isipokuwa kwasababu ya kazi yake na inajumuisha ajali itakayotokea wakati wa kwenda au kurudi kazini;

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Wadhamini ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 6 cha Sheria;

"Daktari" maana yake ni Daktari aliyesajiliwa ambaye ameteuliwa kwa ajili ya kufanya tathmini ya majeraha, ajali au maradhi yanayotokana na kazi kwa lengo la kulipa fao la kuumia kazini;

"maradhi yanayotokana na kazi" maana yake ni maradhi yaliyoainishwa katika Jadweli la Kwanza la Kanuni hizi au maradhi mengine yatakayothibitishwa na Daktari kuwa yametokana au yametokea katika kutekeleza majukumu ya kazi;

"Mfuko" maana yake ni Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar;

"ulemavu wa muda" maana yake majeraha yaliyopelekea ulemavu wa muda fulani na baadae kurejea kazini kama kawaida;

"ulemavu wa kudumu" maana yake ulemavu uliopelekea kupoteza kiungo cha mwili au kiungo kutoweza kufanya kazi;

"pato la mfanyakazi" maana yake ni mshahara jumuishi wa mfanyakazi kwa mwezi anaolipwa na mwajiri wake;

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar, Nam. 2 ya 2005;

"Skimu" maana yake ni Skimu ya Fidia ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar iliyoanzishwa chini ya kanuni ya 4 ya Kanuni hizi.

SEHEMU YA PILI
KUANZISHWA KWA SKIMU YA FIDIA

Kuanzishwa kwa Skimu.

4.- (1) Kunaanzishwa Skimu ambayo itajulikana kama Skimu ya Fidia ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar.

(2) Skimu itaendeshwa na kusimamiwa na Mfuko katika kutekeleza kazi zilizoelezwa katika Kanuni hizi.

Chanzo cha fedha za Skimu.

5. Chanzo cha Fedha za Skimu ni:

(a) michango itakayolipwa na waajiri chini ya Sheria;

(b) fedha itakayolipwa kama adhabu chini ya masharti ya Sheria;

(c) mapato yanayotokana na uwekezaji wa fedha za Skimu; na

(d) fedha nyengine yoyote itakayopatikana kihalali na Skimu.

Matumizi ya fedha za Skimu.

6. Fedha za Skimu zitatumika kwa:

(a) kulipa mafao;

(b) kugharimia tathmini ya ajali au maradhi ya wafanyakazi kwa lengo la kulipa mafao;

(c) kuimarisha uwepo wa usalama na afya kazini; na

(d) matumizi mengine yoyote ambayo Skimu itafanya kuhusiana au katika kutekeleza kazi chini ya masharti ya Kanuni hizi.

Kazi za Skimu.

7. Kazi za Skimu ni:

(a) kufuatilia kuhusu majeraha, ajali, vifo na maradhi yanayotokana na kazi;

(b) kupokea taarifa za ajali, maradhi yanayotokana na kazi, vifo na malalamiko ya fao la kuumia kazini;

(c) kukusanya michango kutoka kwa waajiri;

(d) kulipa fao la kuumia kazini kwa mujibu wa masharti ya Sheria na Kanuni hizi;

(e) kuweka kumbukumbu na kutunza takwimu na taarifa za ajali, maradhi yanayotokana na kazi, vifo na ulipaji wa mafao;

(f) kuhamasisha uzuiaji wa ajali, maradhi yanayotokana na kazi na vifo;

(g) kufanya maamuzi juu ya jambo lolote linalohusiana na haki ya mafao, hesabu za mapato, kiwango cha ulemavu cha mfanyakazi, kiwango na namna ya ulipaji wa Fao la Kuumia Kazini au kusitisha malipo ya fao la kuumia kazini;

(h) kutoa elimu na kujenga uwelewa kwa umma juu ya fao la kuumia kazini; na

(i) kufanya kazi nyengine zozote ambazo zitaonekana ni muhimu

katika kuimarisha na kufanikisha malengo ya Skimu.

Wajibu wa Mwa-jiri katika Skimu.

8. Kila mwajiri anawajibu wa:

(a) kuwasilisha michango katika Skimu kwa mujibu wa kiwango, utaratibu na muda ulioainishwa chini ya masharti ya Sheria na Kanuni hizi;

(b) kuwasilisha kwa Skimu taarifa au ripoti yoyote ya ajali, maradhi yanayotokana na kazi au kifo cha mfanyakazi na maelezo maalum ya ajali hiyo, maradhi yanayotokana na kazi au kifo katika utaratibu na muda ulioainishwa katika Kanuni hizi; na

(c) kushirikiana na kuisaidia Skimu kwa namna yoyote inayowezekana katika kutekeleza kazi zake zilizoelezwa chini ya masharti ya Kanuni hizi.

SEHEMU YA TATU
HAKI YA FAO LA KUUMIA KAZINI NA UKOKOTOAJI WA MAFAO YANAYOLIPWA NA SKIMU

Haki ya Fao la Kuumia Kazini.

9.-(1) Mfanyakazi anastahiki fao la kuumia kazini kwa mujibu wa masharti ya Kanuni hizi endapo:

(a) amepata majeraha kutokana na ajali, maradhi yanayotokana na kazi au kifo katika kutekeleza majukumu yake ya kazi; na

(b) mchango wa mfanyakazi wa angalau mwezi mmoja umelipwa na mwajiri katika Skimu kabla ya kutokea kwa ajali, maradhi yanayotokana na kazi au kifo.

(2) Bila ya kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, mfanyakazi hatostahiki kupatiwa haki ya fao la kuumia kazini endapo:

(a) mfanyakazi alikuwa anatekeleza kwa makusudi jukumu ambalo halikuwa jukumu la mfanyakazi husika na hakuwa na ruhusa, idhini au maelekezo ya kutekeleza jukumu hilo kulikopelekea ajali, maradhi yanayotokana na kazi au kifo;

(b) kulikuwa na jambo la makusudi lililofanywa na mfanyakazi kusababisha ajali;

(c) katika hali yoyote ile amepata ajali iliyotokana na uzembe au imesababishwa na uzembe wa mfanyakazi mwenyewe;

(d) ajali imetokea kutokana na majanga ya asili au shambulio la kigaidi;

(e) kwa kujua amewasilisha taarifa zisizo sahihi au za kupotosha; au

(f) amekataa bila ya sababu au kwa dharau ya maksudi kupata msaada wa matibabu kutokana na ajali au maradhi yanayotokana na kazi.

(3) Endapo mfanyakazi amepata ajali chini ya aya (a), (b) na (c) ya kanuni ndogo ya (2) ya kanuni hii, fao la kuumia kazini litalipwa endapo:

(a) ajali imemsababishia ulemavu wa kudumu ulio kamili uliopelekea kutoweza kurejea kazini au kubakia kitandani milele; au

(b) mfanyakazi amefariki kutokana ajali hiyo na ameacha wategemezi.

(4) Bila ya kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, fao la kuumia kazini litakalolipwa kwa mfanyakazi halitajumuisha msaada wa matibabu au gharama za matibabu kwa ajili ya matibabu ya mfanyakazi husika.

(5) Endapo Mfanyakazi alikuwa katika juhudi za kuokoa mali za mwajiri wake au kumuokoa mtu mwengine yeyote aliyemo katika eneo la kazi, itahesabiwa kuwa ajali hiyo imetokea katika kutekeleza majukumu ya kazi bila ya kujali kuwa mfanyakazi alikuwa anafanya hivyo bila ya maelekezo ya mwajiri.

Mafao yanayo-lipwa na Skimu.

10.-(1) Skimu italipa fao la kuumia kazini kwa kila mfanyakazi anayepata majeraha kutokana na ajali, maradhi yanayotokana na kazi au kifo kilichotokea kutokana na kutekeleza majukumu yake ya kazi.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, fao la kuumia kazini litajumuisha:

(a) fao la kupatwa na majeraha na ulemavu wa muda;

(b) fao la ulemavu wa kudumu ambao haumzuii mfanyakazi kurejea kazini;

(c) fao la ulemavu wa kudumu ambao unamzuia mfanyakazi kurejea kazini;

(d) fao la mhudumu wa mfanyakazi mgonjwa asiyejiweza na asiyeweza kurejea kazini; na

(e) fao la kifo.

(3) Fao la kuumia kazini litalipwa baada ya mfanyakazi kupona na kurejea kazini isipokuwa kama ajali au maradhi yanayotokana na kazi

yatasababisha kutoweza kurejea tena kazini au kifo cha mfanyakazi husika.

Fao la kupatwa na majeraha na ulemavu wa muda.

11.-(1) Endapo mfanyakazi amepata majeraha kutokana na ajali au maradhi yanayotokana na kazi wakati anatekeleza majukumu yake, na majeraha hayo yamesababisha ulemavu wa muda, mfanyakazi huyo atalipwa fao la kupatwa na majeraha na ulemavu wa muda.

(2) Fao la kupatwa na majeraha au ulemavu wa muda litakokotolewa kulingana na:

(a) majeraha baada ya kutokea kwa ajali au maradhi yanayotokana na kazi; na

(b) kwa kuzingatia idadi ya siku ambazo mfanyakazi hakuweza kuhudhuria kazini kwa ruhusa ya Daktari.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (2) ya kanuni hii, fao la kupatwa na majeraha na ulemavu wa muda litakuwa sawa na asilimia hamsini ya pato la siku la mfanyakazi wakati wa ajali likizidishwa na idadi ya siku ambazo mfanyakazi hakuhudhuria kazini kwasababu ya ulemavu wa muda.

(4) Endapo mfanyakazi hayupo tena kazini katika kipindi ambacho maradhi yanayotokana na kazi yamegundulika, pato la mfanyakazi huyo litaamuliwa na Mkurugenzi Mwendeshaji kwa kuzingatia pato ambalo mfanyakazi alikuwa anapata kabla hajaondoka kazini.

(5) Maombi ya fao la kupatwa na majeraha na ulemavu wa muda yatazingatiwa ikiwa mfanyakazi hakuweza kuhudhuria kazini kuanzia siku tatu na kipindi kisichozidi miezi arobaini na nane kwa ruhusa ya Daktari.

(6) Endapo mfanyakazi hataweza kuhudhuria kazini zaidi ya kipindi cha miezi arobaini na nane, kutokana na kupatwa na majeraha au maradhi yanayotokana na kazi, atachukuliwa kuwa amepata ulemavu wa kudumu.

Fao la ulemavu wa Kudumu ambao haumzuii mfanyakazi kurejea kazini.

12.-(1) Endapo mfanyakazi amepata majeraha kutokana na ajali au maradhi yanayotokana na kazi wakati anatekeleza majukumu yake, na majeraha hayo yamesababisha kupoteza kiungo au viungo ambayo hayamzuii mfanyakazi kurejea kazini, mfanyakazi huyo atalipwa Fao la Ulemavu wa kudumu ambao haumzuii mfanyakazi kurejea kazini.

(2) Fao la ulemavu wa kudumu ambao haumzuii mfanyakazi kurejea kazini litakuwa sawa na asilimia ya ulemavu wa kiungo husika ikizidishwa na miezi arobaini na nane ya pato la mwezi la mfanyakazi kwa mujibu wa masharti ya Kanuni hizi.

(3) Katika kulipa fao la ulemavu wa kudumu ambao haumzuii mfanyakazi kurejea kazini, kutokufanya kazi kwa kiungo kutazingatiwa sawa na kupoteza kiungo.

Fao la ulemavu wa kudumu ambao unamzuia mfanyakazi kurejea kazini.

13.-(1) Endapo mfanyakazi amepata majeraha kutokana na ajali au maradhi yanayotokana na kazi wakati anatekeleza majukumu yake, na majeraha hayo yamesababisha ulemavu wa kudumu unaomzuia mfanyakazi kurejea kazini, mfanyakazi huyo atalipwa Fao la Ulemavu wa kudumu ambao unamzuia mfanyakazi kurejea kazini.

(2) Fao la ulemavu wa kudumu ambao unamzuia mfanyakazi kurejea kazini litakuwa sawa na pato la miezi arobaini na nane la mfanyakazi husika.

Fao la mhudumu wa mfanyakazi mgonjwa ambaye asiyejiweza na asiyeweza kurejea kazini.

14.-(1) Endapo mtu wa karibu au mtu mwengine yeyote anamuhudumia mfanyakazi aliyepata ulemavu wa kudumu ambaye hawezi kujifanyia huduma muhimu za kimaisha bila ya kuwa na mhudumu, atalipwa fao la mhudumu wa mfanyakazi mgonjwa ambaye asiyejiweza na asiyeweza kurejea kazini.

(2) Jina la Mhudumu alietajwa katika kanuni ya (1) ya kanuni hii litawasilishwa kwa Mkurugenzi Mwendeshaji na mfanyakazi husika ambae anahitaji mhudumu.

(3) Kiwango cha fao la mtu anayemuhudumia mfanyakazi aliyepata ulemavu wa kudumu asiyejiweza kujihudumia mahitaji yake muhimu ya kimaisha kutokana na ulemavu litakuwa robo ya kiwango cha fao la ulemavu wa kudumu alicholipwa mfanyakazi husika na litalipwa kwa mkupuo mara moja tu.

Fao la kifo kwa wategemezi wa mfanyakazi.

15.-(1) Wategemezi wa mfanyakazi aliyefariki kutokana na ajali kazini, maradhi yanayotokana na kazi au maradhi mengine yanayotokana na kazi yaliyothibitishwa na Daktari, watalipwa fao la kifo kwa kwa mujibu wa masharti ya Kanuni hizi.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, fao la kifo litalipwa kwa wategemezi wa mfanyakazi aliyefariki mara moja tu kwa mkupuo ambalo litakuwa sawa na pato la miezi arobaini na nane la mfanyakazi aliyefariki.

(3) Fao la kifo litakalolipwa chini ya kanuni ndogo ya (2) ya kanuni hii, litakuwa sehemu ya mali ya mfanyakazi husika na litalipwa kwa wategemezi wa mfanyakazi aliyefariki kupitia taasisi inayohusika na masuala ya mirathi.

Fao la kuumia kazini kwa wanafunzi wanaofanya mafunzo kwa vitendo.

16.-(1) Skimu italipa fao la kuumia kazini kwa wanafunzi watakaopata ajali au maradhi yanayotokana na kazi katika sehemu ya kazi wanaofanya mafunzo kwa vitendo kwa taasisi au chuo ambacho ni Mwanachama wa Mfuko.

(2) Ukokotoaji wa fao la kuumia kazini kwa wanafunzi watakaopata ajali au maradhi yanayotokana na kazi katika sehemu ya kazi wanaofanya mafunzo kwa vitendo kwa taasisi au chuo ambacho ni Mwanachama wa Mfuko utafanywa kwa kuzingatia au kwa kigezo cha kima cha chini cha

mshahara wa Serikali.

(3) Utaratibu wa ombi la fao hili kwa wanafunzi hao utakuwa sawa na utaratibu wa wafanyakazi.

Ajali wakati wa kwenda na kurejea kazini.

17. Ajali itakayotokea wakati wa kwenda au kurejea kazini moja kwa moja itahesabiwa kuwa imetokea katika kutekeleza majukumu yake ya kazi.

Ajali wakati wa mafunzo au huduma za dharura.

18. Kwa madhumuni ya Kanuni hizi, ajali itazingatiwa kuwa ajali kazini, endapo mfanyakazi:

(a) alikuwa katika mafunzo ya kutoa huduma ya kwanza, huduma za kusafirisha wagonjwa, uokozi, kuzima moto au huduma nyengine zozote za dharura; au

(b) alihusika katika kazi au mazingira ya mwajiri ya utoaji huduma ya kwanza, huduma za kusafirisha wagonjwa au uokozi, kuzima moto au huduma nyengine zozote za dharura katika eneo lake la kazi.

Ajali iliyotokea au maradhi yaliyopatikana nje ya Zanzibar.

19. Endapo mwajiri anaendesha shughuli zake Zanzibar na mfanyakazi wake ambaye kwa kawaida anafanya kazi Zanzibar amepata ajali au maradhi yanayotokana na kazi wakati anafanya kazi nje ya Zanzibar, mfanyakazi huyo atastahiki kulipwa fao la kuumia kazini kana kwamba ajali hiyo imempata au maradhi hayo yamempata akiwa Zanzibar.

Ajali au maradhi yaliyotokea ndani ya Zanzibar.

20.-(1) Endapo mwajiri anaendesha shughuli zake nje ya Zanzibar, na mfanyakazi wake ambaye kwa kawaida anafanya kazi nje ya Zanzibar amepata ajali au maradhi yanayotokana na kazi wakati anafanya kazi akiwa Zanzibar, mfanyakazi huyo hatastahiki kulipwa fao la kuumia Kazini kutoka katika Skimu, isipokuwa kama kutakuwa na mchango uliolipwa na mwajiri katika Skimu kabla ya kutokea ajali, maradhi yanayotokana na kazi au kifo kwa mfanyakazi husika.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, mfanyakazi ambaye anafanya kazi Zanzibar kwa kipindi cha zaidi ya miezi sita, atazingatiwa kuwa ameajiriwa na mwajiri Zanzibar na mwajiri wake atawasilisha michango katika Skimu.

(3) Endapo mfanyakazi anastahili kulipwa fao la kuumia kazini chini ya masharti ya Kanuni hizi anaweza kuomba fao la kuumia kazini au fao linalofanana na hilo chini ya Sheria zinazotumika Tanzania Bara, mfanyakazi huyo ataomba na kulipwa fao hilo katika Skimu au Mfuko mmoja tu Tanzania Bara au Zanzibar ambalo litakuwa na kiwango kikubwa.

(4) Endapo mfanyakazi ambaye kwa kawaida anafanya kazi Zanzibar atapata ajali au maradhi yanayotokana na kazi wakati anafanya kazi baharini, mfanyakazi huyo atastahili kulipwa fao la kuumia kazini kana

kwamba ajali hiyo imempata au maradhi hayo yamempata akiwa Zanzibar.

Fao la kuumia kazini kutokupunguzwa au kunyimwa.

21. Bila ya kuathiri masharti ya Sheria nyengine yoyote, fao la kuumia kazini halitonyimwa, kuwekwa rehani au kutumika kwa ajili ya kutekeleza hukumu au amri ya Mahakama au kulipia madeni ya mfanyakazi anayestahiki kulipwa fao hili.

Malipo ya mafao kwa mtu ambaye alishawahi kulipwa.

22. Endapo mfanyakazi amepata ajali au maradhi yanayotokana na kazi na kufanyiwa malipo, na baadae ikatokea kifo chake na kuthibitishwa kwamba kifo hicho kinatokana na ajali au maradhi yanayotokana na kazi ambapo alishawahi kulipwa awali au kufanyika mapitio ya asilimia ya ulemavu, Mkurugenzi Mwendeshaji atalipa fao la kifo kwa kukata kiwango cha malipo kilicholipwa mwanzoni kwa mfanyakazi husika kama ilivyoelezwa katika Kanuni hizi.

Katazo la kukata au kupunguza mshahara.

23. Mwajiri hatapunguza au kukata kiwango chochote cha mshahara wa mfanyakazi katika hali yoyote ile kumfidia mwajiri moja kwa moja au vyenginevyo kiwango chochote ambacho mwajiri anapaswa kulipa au kuchangia chini ya masharti ya Sheria au Kanuni hizi.

Kuacha au kusamehe fao la kuumia kazini.

24. Mkataba wowote ambao mfanyakazi ataingia kwa lengo la kuacha au kusamehe fao la kuumia kazini chini ya masharti ya Kanuni hizi utakuwa batili.

Vitisho na kulazimisha kunakatazwa.

25. Mtu yeyote asimtishe, kulazimisha au kumshawishi mfanyakazi kufanya jambo lolote ambalo litampelekea kunyimwa au kupoteza haki yake ya fao la kuumia kazini chini ya masharti ya Kanuni hizi.

Msaada wa matibabu na mazishi.

26.-(1) Kila mwajiri anawajibu na jukumu la kutoa msaada wa matibabu pamoja na kulipia gharama za matibabu ya mfanyakazi wake atakayepata majeraha yanayotokana na ajali au maradhi yanayotokana na kazi kabla ya mfanyakazi kulipwa fao la kuumia kazini.

(2) Mwajiri atatoa msaada wa matibabu au atalipia gharama za matibabu ya mfanyakazi wake atakayepata majeraha yanayotokana na ajali au maradhi yatoyokana na kazi kwa kipindi kisichopungua miaka miwili kutoka siku ya ajali au siku ya kugunduliwa kwa maradhi yanayotokana na kazi kwa mfanyakazi husika.

(3) Kila mwajiri ana jukumu la kutoa msaada wa mazishi au gharama za mazishi ya mfanyakazi wake aliyefariki kutokana na ajali au maradhi yanayotokana na kazi.

Nyongeza ya Kiwango cha Mafao.

27.-(1) Waziri, kwa kushauriana na Bodi, anaweza kupitia Gazeti Rasmi kuongeza kiwango cha mafao yanayolipwa chini ya Kanuni hizi kwa kiwango ambacho ataona kinafaa.

(2) Nyongeza ya kiwango cha mafao haitofanywa na Waziri isipokuwa baada ya kufanyika Tathmini ya Uhimilivu wa Skimu, na Tathmini ya Uhimilivu lazima ioneshe kuwa kuna uwezekano wa kuongeza

kiwango cha mafao bila ya kuathiri uendelevu wa Skimu.

Mfumo wa Malipo.

28.-(1) Malipo ya fao la kuumia kazini yatafanywa kwa njia ya mkupuo mara moja tu katika hesabu ya Benki ya Mwanachama kwa mujibu wa taratibu za ulipaji wa Mafao ya Mfuko.

(2) Endapo mwanachama amefariki, fao la kifo litalipwa kupitia:

(a) hesabu za Benki za Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Zanzibar kwa mfanyakazi Muislamu; na

(b) kwa Mkurugenzi anayehusika na Usajili wa Mali na Biashara Zanzibar kwa mfanyakazi asiyekuwa Muislamu.

SEHEMU YA NNE
UTARATIBU WA MAOMBI YA FAO LA KUUMIA KAZINI

Taarifa ya ajali.

29.-(1) Mfanyakazi au mtu mwengine yeyote kwa niaba ya mfanyakazi anatakiwa kutoa taarifa ya maandishi au ya mdomo kwa mwajiri wake au kwa Mkurugenzi Mwendeshaji juu ya ajali iliyompata ndani ya siku saba baada ya ajali kutokea.

(2) Endapo mfanyakazi ameshindwa kutoa taarifa kwa mwajiri wake kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, haitazuia haki yake ya fao la kuumia kazini ikiwa itathibitishwa kuwa kulikuwa na sababu za msingi zilizopelekea kushindwa kutoa taarifa katika muda uliopangwa au mwajiri alikuwa na taarifa juu ya ajali hiyo.

(3) Mwajiri baada ya kupokea taarifa ya ajali kutoka kwa mfanyakazi au kuwa na taarifa kwamba ajali imetokea, ndani ya siku saba atamjuulisha Mkurugenzi Mwendeshaji kupitia Fomu SSF. 17 iliyoainishwa katika Jadweli la Pili la Kanuni hizi.

(4) Mwajiri, kwa ombi la mfanyakazi au mtegemezi wa mfanyakazi, atampatia mfanyakazi au mtegemezi wa mfanyakazi nakala ya taarifa ya ajali iliyotolewa kwa Mkurugenzi Mwendeshaji kuhusiana na taarifa ya ajali.

Taarifa ya maradhi yanayotokana na kazi.

30.-(1) Mfanyakazi au mtu mwengine yeyote kwa niaba ya mfanyakazi, ndani ya siku kumi na nne baada ya uthibitisho wa Daktari kuwa mfanyakazi amepata maradhi yanayotokana na kazi, atatoa taarifa kwa mwajiri au mwajiri wa mwisho wa mfanyakazi.

(2) Mwajiri, ndani ya siku saba baada ya kupokea taarifa ya uthibitisho wa Daktari kuwa mfanyakazi amepata maradhi yanayotokana na kazi, atatoa taarifa kwa Mkurugenzi Mwendeshaji kupitia Fomu SSF. 17 iliyoainishwa katika Jadweli la Pili la Kanuni hizi.

Taarifa ya kifo cha mfanyakazi.

31.-(1) Mtegemezi, ndani ya siku thelathini baada ya kifo cha mfanyakazi kilichotokana na ajali au maradhi yanayotokana na kazi, atatoa

taarifa kwa mwajiri au mwajiri wa mwisho wa mfanyakazi.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, mwajiri ndani ya kipindi cha siku saba baada ya kupokea taarifa ya kifo cha mfanyakazi kutoka kwa wategemezi, atatoa taarifa kwa Mkurugenzi Mwendeshaji kupitia Fomu SSF. 17 iliyoainishwa katika Jadweli la Pili la Kanuni hizi.

Ombi la fao la kuumia kazini.

32.-(1) Mfanyakazi au mtu mwengine yeyote kwa niaba ya mfayakazi ataomba fao la kuumia kazini kwa Mkurugenzi Mwendeshaji kwa kujaza Fomu SSF. 18 iliyoainishwa katika Jadweli la Pili la Kanuni hizi.

(2) Endapo mfanyakazi amefariki kutokana na ajali au maradhi yanayotokana na kazi, ombi la fao la kuumia kazini litawasilishwa na wategemezi wake ndani ya siku kumi na nne baada ya kuwasilisha taarifa ya kifo cha mfanyakazi kwa mwajiri wake.

(3) Katika kuwasilisha ombi chini ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, mfanyakazi au mtu mwengine yeyote kwa niaba ya mfanyakazi atawasilisha vielelezo vifuatavyo;

(a) nakala ya kadi ya uanachama ya Mfuko;

(b) karatasi ya kuhudhuria hospitali;

(c) cheti cha kifo iwapo ajali au maradhi yamesababisha kifo;

(d) ripoti ya daktari au ripoti ya matibabu;

(e) fomu ya PF3 au PF 90;

(f) taarifa ya Bodi ya madaktari (ikiwa ni maradhi yanayotokana na kazi au ulemavu wa kudumu ambao mfanyakazi hawezi kurejea kazini); na

(g) taarifa nyengine yoyote ambayo itakuwa inafaa.

Kupokelewa kwa ombi la fao.

33.-(1) Mkurugenzi Mwendeshaji, baada ya kupokea maombi ya mafao na vielelezo vyake, atafanya uhakiki wa usahihi wa ombi hilo na vielelezo vilivyoambatishwa na ombi hilo.

(2) Endapo ombi lililowasilishwa chini ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii ni sahihi, Mkurugenzi Mwendeshaji atatoa Fomu SSF. 19 iliyoainishwa katika Jadweli la Pili la Kanuni hizi ili iweze kujazwa na Daktari.

(3) Mkurugenzi Mwendeshaji anaweza kuomba ushahidi mwengine wowote wa ulemavu wa muda, endapo kwa maoni yake mazingira ya kesi hiyo yanaruhusu na ushahidi huo wa ziada utajumuisha taarifa na utathibishwa katika namna itakavyoelezwa na Mkurugenzi Mwendeshaji.

(4) Endapo ombi lililowasilishwa na vielelezo vyake lina makosa au halijitoshelezi, Mkurugenzi Mwendeshaji, ndani ya siku tano za kazi baada ya kutambua kuwa ombi lina makosa au halijitoshelezi, anaweza kumtaka mfanyakazi au mtu mwengine yeyote kwa niaba ya mfanyakazi kuwasilisha taarifa za ziada kwa kadri atakavyoona.

Tathmini ya ajali au maradhi.

34.-(1) Kwa madhumuni ya kulipa fao lililoainshwa katika Kanuni hizi, Daktari anajukumu la kufanya tathmini ya kiwango cha majeraha au ulemavu au maradhi yanayotokana na kazi au kifo kwa kujaza fomu SSF. 19 iliyoainishwa katika Jadweli la Pili la Kanuni hizi.

(2) Kutakuwa na Daktari katika kila hospitali ya Wilaya atakayeteuliwa na Wa[illegible]kwa kushauriana na Waziri anayehusika na masuala ya Afya Zanzibar.

(3) Katika kutathmini kiwango cha ulemavu wa kudumu na maradhi chini ya Kanuni hizi, Daktari ataongozwa na viwango vya asilimia vilivyoainishwa katika Jadweli la Tatu la Kanuni hizi.

(4) Daktari, kupitia fomu iliyoainishwa katika kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, ataeleza kiwango cha majeraha au ulemavu ambao umemfanya mfanyakazi kuwa na majeraha au ulemavu wa muda na atainisha kipindi kilichomfanya mfanyakazi kushindwa kufanya kazi kutokana na majeraha au ulemavu.

(5) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii, Daktari ndani ya kipindi kisichozidi siku tatu baada ya kumfanyia tathmini mfanyakazi aliyepata ajali kazini au aliyepata maradhi yanayotokana na kazi, atawasilisha kwa Mkurugenzi Mwendeshaji fomu ya tathmini ya ajali au maradhi.

Kukubaliwa au kukataliwa kwa fomu ya ombi au fomu ya tathmini.

35. Mkurugenzi Mwendeshaji anaweza kuirejesha fomu ya ombi au fomu ya tathmini ya ulemavu au maradhi endapo:

(a) atagundua kuwa imejazwa kimakosa;

(b) haikujazwa kikamilifu; au

(c) imejazwa bila ya kuzingatia masharti ya Kanuni hizi.

Ukokotoaji wa fao la kuumia kazini.

36.-(1) Ukokotoaji wa fao la kuumia kazini utafanywa baada ya Mkurugenzi Mwendeshaji kulikubali na kuliridhia ombi lililowasilishwa na mwajiri, mfanyakazi au mtu mwengine yeyote kwa niaba ya mfanyakazi kwa mujibu wa utaratibu ulioainishwa katika Kanuni hizi.

(2) Endapo mfanyakazi amepata ajali mbili au zaidi zilizofuatana ambazo zinapaswa kulipwa fao la kuumia kazini chini ya masharti ya Kanuni hizi, atalipwa kwa ajali moja iliyokuwa kubwa au iliyompa kiwango

kikubwa cha ulemavu.

(3) Endapo mfanyakazi amepata ajali itakayopelekea majeraha na ulemavu wa kudumu ambao haukumzuia kurejea kazini atalipwa mafao yote mawili.

Kupitwa na muda kwa ombi la fao.

37.- (1) Haki ya kustahiki fao la kuumia kazini kutokana na ajali au maradhi yanayotokana na kazi itapitwa na wakati iwapo ajali au maradhi yanayotokana na kazi haikutolewa taarifa kwa Mkurugenzi Mwendeshaji ndani ya muda wa miezi sita baada ya tarehe ya kutokea kwa ajali au kugundulika kwa maradhi yanayotokana na kazi au kifo.

(2) Kwa madhumuni ya kanuni hii, kupata maradhi yanayotokana na kazi itachukuliwa kuwa ni tarehe ambayo Daktari amegundua maradhi hayo kwa mara ya kwanza na kumjuulisha mfanyakazi juu ya kugundulika na maradhi hayo au tarehe nyengine ya mapema kama Mkurugenzi Mwendeshaji atakavyoweza kuamua.

SEHEMU YA TANO
MASHARTI YA FEDHA

Hesabu za Skimu.

38. Skimu itaweka kumbukumbu na vitabu vya hesabu vya kila mwaka wa fedha vitakavyoonesha taarifa za mapato na matumizi ya Skimu pamoja na mali na madeni ya skimu.

Bajeti ya Skimu.

39. Mkurugenzi Mwendeshaji katika kipindi cha miezi tatu kabla ya kumalizika mwaka wa fedha au katika kipindi kingine chochote kama itakavyoelekezwa na Bodi, atawasilisha katika Bodi bajeti itakayoonesha makadirio ya mapato na matumizi ya Skimu kwa ajili kuidhinishwa na Bodi.

Ripòti za mwaka za Skimu.

40. Ndani ya kipindi cha miezi sita baada ya kila mwisho wa mwaka, Skimu itawasilisha kwa Bodi ripoti ya mwaka itakayoonesha shughuli za Skimu kwa mwaka huo wa fedha.

SEHEMU YA SITA
MASHARTI MENGINEYO

Makosa na Adhabu.

41.-(1) Mtu yeyote ambaye:

(a) ameshindwa kulipa au kuwasilisha michango au faini katika Skimu kwa wakati;

(b) ameshindwa kutoa nyaraka au taarifa inayotakiwa kutolewa chini ya Kanuni hizi;

(c) amepunguza au amekata kutoka kwa mfanyakazi kiasi chochote kuhusiana na michango katika Skimu;

(d) amekwepa kulipa michango yeye mwenyewe au mtu mwengine yeyote;

(e) ametoa taarifa za uongo;

(f) amewasilisha au kusababisha kuwaslishwa nyaraka au taarifa ambayo anajua kwamba taarifa hiyo ni ya uongo;

(g) amejipatia isivyohalali fao la kuumia kazini yeye mwenyewe au kwa mtu mwengine;

(h) amezuia au kumshambulia mfanyakazi yeyote wa Skimu katika kutekeleza majukumu yake; au

(i) ameshindwa kutii na kufuata ipasavyo masharti ya Kanuni hizi;

ametenda kosa na akitiwa hatiani atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Moja za Kitanzania au kifungo kisichopungua mwaka mmoja au adhabu zote mbili kwa pamoja.

(2) Mahakama itakayomtia hatiani kwa kosa lililoainishwa katika aya (a) na (d) ya kanuni hii itaamuru mtiwa hatiani huyo kulipa katika Skimu kiwango cha michango anachodaiwa pamoja na adhabu siku ya tarehe ya kutiwa hatiani.

Tathmini ya uhimilivu wa Skimu.

42. Bodi itahakikisha kuwa Skimu inafanyiwa tathmini ya uhimilivu kila baada ya kipindi cha miaka mitatu au katika kipindi kingine chochote ambacho Bodi itaona kuwa inafaa ili kupima uhimilivu wa Skimu kutekeleza majukumu yake pamoja na rasilimali na madeni.

Ukaguzi wa sehemu za kazi.

43.-(1) Wakaguzi wa Idara ya Usalama na Afya Kazini wataendelea kuwa na jukumu la kukagua sehemu za kazi kuhusiana na mambo yanayohusiana na masharti ya afya na usalama kazini.

(2) Katika kufanya maamuzi juu ya maombi ya fao la kuumia kazini, Mkurugenzi Mwendeshaji atazingatia ripoti za wakaguzi wa afya na usalama kazini kuhusiana na sehemu ya kazi ambayo mfanyakazi amepata majeraha, ajali au maradhi yanayotokana na kazi.

(3) Endapo ajali imetokea kwasababu mwajiri ameshindwa kuchukua hatua muwafaka kulinda au kuweka mazingira salama ya kazi, Skimu haitakuwa na jukumu la kulipa fao la kuumia kazini kwa mfanyakazi yeyote isipokuwa madai ya malipo hayo yatalipwa na mwajiri na gharama nyengine ambazo Skimu imeingia chini ya masharti ya Kanuni hizi.

Kupata taarifa za Skimu.

44. Mfanyakazi au mtegemezi wa mfanyakazi aliyefariki ana haki ya kupata taarifa au nyaraka yoyote iliyopo katika Skimu inayohusiana na ajali, majeraha, maradhi yanayotokana na kazi kwa kadri ya hali itakavyokuwa.

JADWELI

JADWELI LA KWANZA

MARADHI YANAYOTOKANA NA KAZI YANAYOSTAHILI KUFIDIWA

[Chini ya kanuni ya 3]

MAELEZO YA MARADHI AU JERAHA	AINA YA KAZI
I. MARADHI MAKUBWA AU MAKUBWA KIASI YANAYOTOKANA NA SUMU YA METALI AU MCHANGANYIKO WAKE.	
1. Ugonjwa unaotokana na aseniki au aseniki au na mchanganyiko wake.	Kazi inayohusisha kuathirika na mchanganyiko wake.
2. Ugonjwa unaotokana na beriliamu au kutokana na mchanganyiko wake	Kazi inayohusisha kuathirika beriliamu au mchanganyiko wake.
3. Ugonjwa unaotokana na kadmian au kutokana na mchanganyiko wake.	Kazi inayohusisha kuathirika kadmian au mchanganyiko wake.
4. Ugonjwa unaotokana na kromiamu kromiamu au mchanganyiko wake.	Kazi inayohusisha kutokana na au mchanganyiko wake.
5. Ugonjwa unaotokana na risasi au kutokana na mchanganyiko wake.	Kazi inayohusisha kuathirika risasi au mchanganyiko wake.
6. Ugonjwa unaotokana na manganizi kutokana na au mchanganyiko wake.	Kazi inayohusisha kuathirika manganizi au mchanganyiko wake.
7. Ugonjwa unaotokana na zebaki au kutokana na mchanganyiko wake.	Kazi inayohusisha kuathirika zebaki au mchanganyiko wake.
8. Ugonjwa unaotokana na metali nyengine yoyote au mchanganyiko wake.	Kazi inayohusisha kuathirika kutokana na metali nyengine yoyote au mchanganyiko wake.
II. MARADHI MAKUBWA AU MAKUBWA KIASIYANAYOTOKANA NA METALI NYENGINE.	
9. Ugonjwa unaotokana na "acrylamide monomer" au mchanganyiko wake.	Kazi inayohusisha kuathirika kutokana na "acrylamide monomer" au mchanganyiko wake.
10. Ugonjwa unaotokana na benzini au mchanganyiko wake.	Kazi inayohusisha kuathirika kutokana na kenzini au mchanganyiko wake.
11. Ugonjwa unaotokana na amino-	Kazi inayohusisha kuathirika mitro-au

chloro- nitrochlor-derivatives ya benzini au mchanganyiko wake.	kutokana na amino-chro-, au nitrochlor-derivatives yabenzini mchanganyiko wake.
12. Ugonjwa unaotokana na carbon disulphide.	Kazi inayohusisha kuathirika kutokana na carbon disulphide.
13. Ugonjwa unaotokana na halogenated aliphatic & aromatic (hydrocarbons) compounds.	Kazi inayohusisha kuathirika kutokana na halogenated & aromatic (hydrocarbons) compounds.
14. Ugonjwa unaotokana na diethlene dioxide (dioxan).	Kazi inayohusisha kuathirika kutokana na moshi au mvuke wenye diethylene dioxide.
15. Ugonjwa unaotokana na dinitrophenol dinitrophenol dioxide au mchanganyiko wake au substituted dinitrophenols au chumvi za viini hivyo.	Kazi inayohusisha kuathirika na dioxide au mchanganyiko wake au substituted dinitrophenols au chumvi za viini hivyo.
16. Ugonjwa unaotokana na bromidi ya methili.	Kazi inayohusisha kuathirika kutokana na moshi au mvuke kwenye bromidi ya methili.
17. Ugonjwa unaotokana na kaboniki ya nikeli.	Kazi inayohusisha kuathirika kutokana na gesi kaboniki ya nikeli.
18. Ugonjwa unaotokana na moshi wa nitras.	Kazi inayohusisha kuathirika kutokana na moshi wa nitras.
19. Ugonjwa unaotokana na viuadudu.	Kazi inayohusisha kuathirika kutokana na viuadudu.
20. Ugonjwa unaotokana na fosforasi au mchanganyiko wake.	Kazi inayohusisha kuathirika kutokana na fosforasi au mchanganyiko wake.
21. Ugonjwa unaotokana na viyeyushi vya ogani.	Kazi inayohusisha kuathirika kutokana na viyeyushi vya ogani.
22. Ugonjwa unaotokana na trikresili ya fosfeti.	Kazi inayohusisha kuathirika kutokana na moshi au mvuke wa trikresili ya fosfeti.
23. Ugonjwa unaotokana na trifenili ya fosfeti.	Kazi inayohusisha kuathirika kutokana na moshi au mvuke wa trifenili ya fosfeti.
24. Ugonjwa unaotokana na kemikali nyengine yoyote inayotumiwa katika sehemu za kazi na kuathiri viungo au sehemu ya mwili.	Kazi inayohusisha kuathirika kutokana na kemikali zozote nyengine ambazo zimethibitika kisayansi kwamba zinaathiri afya ya binaadamu.

III. MZIO

25. Pumu inayosababishwa na kazi.	Kazi inayohusisha kuathirika kutokana na ajenti za kibaiolojia au kemikali ambazo zimethibitika kisayansi kuwa na mzio katika upumuaji.
26. Ugonjwa wa ngozi unaosababishwa na kazi.	Kazi inayohusisha kuathirika kutokana na ajenti za kibaiolojia au kemikali ambazo zimethibitika kisayansi kuwa zinaleta maradhi ya ngozi.
27. Ugonjwa wowote wenye mzio.	Kazi inayohusisha kuathirika kutokana na ajenti zozote za kibaiolojia au kemikali ambazo zimathibitika kisayansi kuwa zinaleta madhara.

IV. MARADHI YA MAPAFU YANAYOSABABISHWA NA VUMBI

28. Ugonjwa wa nimonia ikiwa ni pamoja na uletwao na asbestos.	Kazi inayohusisha kuathirika ugonjwa kutokana na vumbi la madini ya fibrojeniki ikiwa ni pamoja na asbestos.
29. Maradhi ya mapafu na yanayosababishwa na vumbi oganiki.	Kazi inayohusisha kuathirika kutokana vumbi la oganiki ambalo limethibitika kisanyansi kuwa linaleta maradhi ya mapafu.

V. MARADHI YA KUAMBUKIZA

30. MHIV/UKIMWI.	
31. Ugonjwa wa ankylostomiasis na Geohelminthiasis.	Kazi inayohusisha kuathirika kutokana na minyoo inayopenya katika ngozi na minyoo ya aina nyengine.
32. Kimeta.	Kazi inayohusisha kuathirika kutokana na sufi, nywele, manyoya, ngozi za wanyama, au mabaki mengine ya mnyama aliyepatwa na kimeta.
33. Brusilosi.	Kazi inayohusisha kugusana na wanyama walioathirika na vijidudu vya brusela vya wanyama wafu au sehemu zawanyama hao, au sampuli za maabara au vitu vyengine vyenye

	wadudu wa brusela.
34. "Glanders".	Kazi inayohusisha kugusana na jamii ya wanyama ya punda walioathirika au maiti za wanyama hao.
35. Leptospirosis.	Kazi inayohusisha kuathirika na mkojo au uchafu mwengine unaotokana na mafuta, panya, mbwa, nguruwe au wanyama wa aina ya ngo'mbe walioathirika na vijidudu vya leptospiro.
36. Kichocho.	Kazi inayohusisha kuathirika kutokana na maji yenye makonokono wenye vijidudu vya kichocho.
37. Kifua kikuu.	Kuthibitika kutokana na vijidudu vya kifua kikuu katika kazi ya udaktari, uuguzi, maabara au kufanya kazi katika jamii.
38. Homa ya manjano.	Kazi inayohusu kuwa karibu au kugusa mara kwa mara damu ya binaadamu au vitu vinavyotokana na damu hiyo au vyanzo vyengine vya homa ya manjano inayowapata hasamadaktari au wauguzi wanaofanya kazi hospitalini.
39. Maradhi mengine yoyote yanayoambukiza.	Kazi inayohusisha kuathirika kutokana na viumbe hai vya maradhi vinavyopatikana sehemu za kazi.

VI. ATHARI YA NGUVU ZA ASILI ZA MAUMBILE AU KEMIKALI

40. Bursitis au sub-cutaneousas cellulites inayotokea katika mikono kutokana na msuguo mkubwa au ulioendelea au shinikizo katika kisugudi.	Kazi za nguvu zinazosababishwa mkubwa au unaoendelea au shirikizo katika kisugudi.
41. Brusitis or sub-cutaneous cellulites inayotokea katika magoti kutokana msuguo mkubwa au unaoendelea au shinikizo katika goti.	Kazi za nguvu zinazosababisha msuguo mkubwa au unaoendelea au shinikizo katika goti.
42. Kukakamaa kwa mikono au viganja kutokana na vitendo vinavyofanywa tena na tena.	Vipindi virefu kwa kuandika kwa kutokana na vitendo vinavyofanywa mkono, kupiga taipu au kufanya kazi nyengine inayohusisha vitendo vinavyofanywa tena na tena kwa kutumia vidole, mkono au kiganja.

43. Kuwakwa moto kwa mishipa ya mkono.	Kazi za nguvu zinazohusisha kufanya kitendo tena na tena kwa kutumia mikono au kiganja.
44. Subcutaneous cellulites ya mkono (beat band).	Kazi za nguvu zinazosababisha msuguo mkubwa au unaoendelea wa mkono.
45. Magonjwa mbali mbali yanayotokana na hewa iliyobanwa pamoja na (staggers, bends, chokes, hyperbaric osteonecrosis and other baro-trauma).	Kazi zinazohusisha kufanyakazi katika maeneoyenye hewa iliyobanwa.

VII. SARATANI NA UVIMBE

46. Maotea, dysplasia, uvimbe au Saratani inayosababishwa na kufanya kazi katika mazingira yenye kuleta maradhi ya namna hiyo.	Kazi inayohusisha kuathirika na nguvu za asili za biolojia, kemikali au fizikali ambazo zimethibtishwa kisayansi kwamba zinasababisha maotea, Displasia,uvimbe.

VIII. MARADHI MENGINE

47. Vitiligo ya kazi.	Kazi inayohusisha kuathirika na nguvu za asili za biolojia, kemikali au fizikali zimethibitishwa kisayansi kwamba zinasababisha maotea, displasia, uvimbe au saratani.
48. Maradhi mengine yoyote ambayo yamethibitika kuwa yanatokana na kazi.	Kazi inayohusisha kuathirika kutokana na vitu mbavyo vimethibitishwa kisayansi kuwa vinasababishwa na kazi maradhi hayakutajwa hapo juu

JADWELI LA PILI

MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR

FOMU YA TAARIFA YA AJALI KAZINI, MARADHI AU KIFO
[chini ya kanuni ya 29(3), 30(2) na 31(2)]

SSF 17

(Fomu hii ijazwe na Mwajiri)

A. AINA YA TAARIFA - weka alama ya √ panapohitajika

AJALI KAZINI (jaza sehemu B, C, D, & G		MARADHI KAZINI (jaza sehemu B, C, E & G)		KIFO (Jaza sehemu B, C, F, & G)	

B. TAARIFA ZA MWAJIRI

1. Jina kamili(Wizara/Kampuni/Taasisi).....
2. Taasisi ya Serikali au Binafsi .....
3. Namba ya usajili ya ZSSF .....
4. Anuani .....
5. Nchi .....Mkoa .....
   Wilaya.....Shehia .....
   Mtaa/Kijiji.....
6. Simu ya mezani.....Simu ya mkononi.....
   Tovuti.....Barua pepe.....

C. TAARIFA ZA MWAJIRIWA

1. Jina la kwanza .....Jina la kati .....

2. Jina la mwisho .....

3. Namba ya kitambulisho cha ukaazi /cha Utaifa .....

4. Namba ya uanachama wa ZSSF.....

5. Hali ya Ajira; (kudumu/muda maalum / muda mfupi).....

6. Cheo .....Idara/kitengo .....

Tarehe ya kuzaliwa .....Jinsia .....

7. Hali ya ndoa .....

8. Idadi ya Watoto .....

9. Utaifa .....

10. Mkoa .....Wilaya .....

11. Anuani .....

12. Namba za simu ya mezani .....Namba za simu ya mkononi .....

13. Barua pepe .....

14. Jina la mtu wa karibu .....

15. Namba ya simu ya mtu wa karibu.....

D. MAELEZO YA AJALI KAZINI

1. Tarehe ya Ajali Wakati ilipotokea ajali .....

2. Tarehe ya kutoa taarifa ya ajali kwa mwajiri.....

3. Sehemu ya mwili iliyojeruhiwa .....

4. Mahali ilipotokea ajali; Mtaa, Wadi, Shehia .....

5. Ajali ilitokea kwenye eneo la mwajiri? (Ndio/Hapana).....

6. Kitengo/Idara .....

7. Taja kazi hasa mfanyakazi alikuwa akifanya wakati wa ajali na eleza kwa ufupi mtiririko wa matukio na taja kitu ambacho kilisababisha moja kwa moja jeraha au ajali

.....

.....

8. Mashahidi:

Jina kamili ..... Simu ya mkononi.....

Jina kamili la msimamizi wa kazi .....

simu ya mkononi ..... Kitengo/Idara .....

9. Tarehe ya matibabu ya awali .....

10. Jina la hospitali aliyotibiwa .....

E. MAELEZO YA MARADHI YANAYOTOKANA NA KAZI

1. Tarehe ya kugundulika maradhi .....
2. Aina ya maradhi yaliyogundulika

   Tarehe ya kuripotiwa maradhi kwa mwajiri .....
3. Kitengo/Idara ambayo maradhi hayo yalipatikana .....
4. Eleza kwa ufupi mtiririko wa shughuli zilizohusishwa na maradhi yaliyogunduliwa

.....

.....
5. Jina la Hospitali ambayo maradhi yaligundulika .....
6. Jina la Daktari aliyegundua maradhi .....
7. Namba ya simu ya mkononi. .....

(ambatanisha ripoti za maradhi)

F. MAELEZO YA KIFO

1. Jina la mwakilishi wa Mfanyakazi .....Namba ya simu ya mkononi .....
2. Anuani ya mwakilishi wa mfanyakazi .....
3. Tarehe ya kifo .....
4. Sababu ya kifo,ajali kazini au maradhi yatokanayo na kazi .....
5. Tarehe ya kuripotiwa kifo kwa mwajiri .....
6. Mahali ambapo kifo kimetokea; Mji .....

   Shehia ....., au Mtaa .....
7. Ajali ilitokea katika jengo , eneo la kazi la mwajiri (ndio/hapana) .....
8. Kitengo/Idara .....
9. Eleza Kazi ambayo marehemu alikua akiifanya wakati wa tukio, Elezea kwa ufupi tukio mahsusi ambalo moja kwa moja lilipelekea ajali au maradhi yaliyosababisha kifo chake

.....

.....

10. Jina la Hospitali ambayo kifo kilithibitishwa
.....

11. Jina la Daktari aliethibitisha kifo .....

12. Namba ya simu ya mkononi .....

PART G: UTHIBITISHO WA MWAJIRI

Mimi .....nathibitisha kuwa niliyoyaeleza hapo juu ni kweli kwa kadiri ninavyofahamu na ikithibitika kwamba kuna udanganyifu kuhusiana na taarifa iliyotolewa, hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yangu.

Saini.....

Tarehe.....

Muhuri wa Ofisi.....

MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR
SKIMU YA FIDIA YA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR

FOMU YA OMBI LA FAO LA AJALI KAZINI

[chini ya kanuni ya 32(1)]

SSF. 18

Fomu hii itajazwa na Mwajiriwa au mtu yeyote kwa niaba ya mwajiriwa

A. AINA YA OMBI - weka alama ya (√) panapofaa

Ajali kazini		Maradhi yatokanayo na kazi		Kifo kitokanacho na kazi	

B. MAELEZO YA MWAJIRIWA

1. Jina kamili la mwajiriwa .....
   Mtu wa karibu .....
2. Namba ya usajili ya ZSSF ya mwajiriwa .....
3. Namba ya kitambulisho cha Taifa- NIDA au Zan ID .....
4. Cheo ..... Kitengo/Idara .....
   Pato la mwezi .....
5. Tarehe ya kuzaliwa ..... Jinsia .....
   Hali ya ndoa .....
   Idadi ya Watoto ..... Dini .....
6. Utaifa ..... Mkoa .....

Wilaya .....Shehia .....Mtaa /Kijiji .....

Namba ya Nyumba .....

7. Simu mezani ..... Faksi ..... Simu ya mkononi.....
8. Barua pepe.....

C. MAELEZO YA MWAKILISHI WA MAREHEMU IKIWA MAOMBI YANATOKANA NA KIFO

1. Jina kamili .....

   Anuani.....

2. Nambari ya kitambulisho cha Taifa .....

   Mahusiano na marehemu .....Tarehe ya kuzaliwa .....

   Jinsia ..... Hali ya Ndoa .....

3. Shehia ..... Mtaa/Kijiji ..... Namba ya nyumba .....

4. Simu ya mezani.....Simu ya mkononi .....

5. Barua pepe .....

6. Tarehe, Mahali na Muda wa kifo cha mfanyakazi aliefariki (Ambatanisha nakala ya cheti cha kifo) .....

7. Sababu ya kifo (weka alama √ panapostahiki)

   (a) Ajali kazini ( )

   (b) Maradhi yatokanayo na kazi ( )

8. Jina la Daktari alieufanyia uchunguzi mwili wa marehemu .....

D. TAARIFA ZA MWAJIRI

1. Jina la mwajiri (Wizara/Kampuni/Taasisi) .....

2. Namba ya usajili ya ZSSF.....

3. Nchi ..... Mkoa .....

   Wilaya ..... Shehia .....

   Anuani .....

   Mtaa/Kijiji .....

4. Nambari ya simu ya mezani.....Simu ya mkononi .....

5. Barua pepe .....

E. MAELEZO YA AJALI KAZINI AU MARADHI YATOKANAYO NA KAZI

i. Tarehe ya kuwasilishwa taarifa ya ajali kazini au maradhi kwa mwajiriwa

ii. Majeraha yaliyosababishwa na ajali kazini au maradhi yatokanayo na kazi aliyoyapata .....
.....

iii. Ulijuaje kuwa unaugua maradhi yatokanayo na kazi?

Kufanya vipimo		Kufuatilia kutokana na maradhi		Mengineyo	

Ikiwa mengineyo ainisha .....

F. HISTORIA YA AJIRA: (ijazwe ikiwa ni kesi ya maradhi yatokanayo na kazi)

i. Mwajiri wa sasa

Nam.	Cheo (anza na cheo cha sasa)	Idara	Shughuli iliyokuwa ikifanywa	Muda	
				Kuanzia	Hadi
1.					
2.					
3.					

(Ambatanisha vyeti vinavyothibitisha)

ii. Waajiri wa zamani (ikiwa wapo)

Nam.	Cheo	Mwajiri	Idara	Shughuli iliyokuwa ikifanywa	Muda	
					Kuanzia	Hadi
1.						
2.						
3.						

(Ambatanisha vyeti vinavyothibitisha)

G. HALI YA SASA YA MUAJIRIWA KIAFYA

1.	**Hali ya afya**	Amemaliza matibabu na amepona	Anahudhuria hospitali /kliniki maalum	Amepata ulemavu wa kudumu kwa kupoteza au kutofanyakazi kiungo cha mwili	Amerejea kazini kwa kuendelea na kazi
	Weka alama √ panapofaa				
2.	**Ulemavu**	Amelazwa	Ameshindwa kwenda kazini	Kazi nyepesi	Amepata ulemavu wa jumla yupo kitandani
	Idadi ya siku				

Kwa ufuatiliaji wa matibabu yanayoendelea:

1. Jina na anuani ya mtoa huduma ya afya (Hospitali/Zahanati) .....
.....

2. Jina, anuani na namba ya simu ya Daktari .....

H. Je, uliwahi kulipwa fao lolote linalohusiana na ajali kazini? Ndio/hapana
....

i. Ikiwa ndio ulilipwa fao la aina gani? .....

ii. Ni nani alilipa fidia hiyo? mfano ZSSF .....

iii. Fidia hiyo ililipwa lini? .....

(ambatanisha hati zifaazo)

ITHIBATI YA MWAJIRIWA AU MTU MWENGINE KWA NIABA YA MWAJIRIWA

I, Mimi ..... nathibitisha kuwa niliyoyasema hapo juu ni ya kweli kwa mujibu ya uelewa yangu

Jina .....

Saini .....

Tarehe .....

ITHIBATI YA MWAJIRI

I, Mimi ..... nathibitisha kuwa niliyoyasema hapo juu ni ya kweli kwa mujibu ya uelewa yangu

Jina .....

Saini .....Tarehe .....

NB: Mwajiri lazima awasilishe ripoti ya uchunguzi wa ajali au maradhi yanayotokana na kazi.

Kwa matumizi ya ZSSF tu

Imepokelewa na .....

Jina la Afisa	Cheo	Tarehe	Saini

MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR
SKIMU YA FIDIA YA MFUKO WA HIFADHI YA JAMII ZANZIBAR

FOMU YA TATHMINI

[Chini ya kanuni ya 34(1)]

SSF. 19

Fomu hii inajazwa na Daktari

A. TAARIFA ZA MWAJIRIWA

1. Jina la kwanza ..... Jina la kati.....

   Jina la mwisho .....

2. Namba ya usajili wa ZSSF .....

3. Namba ya faili la matibabu.....Cheo.....

4. Jina la mwajiri (Taasisi).....Namba ya usajili wa ZSSF.....

B. TAARIFA ZA MTOA HUDUMA)

Namba	Jina La Mtoa Huduma	Anuani	Mkoa/Wilaya
1.			
2.			
3.			

C. TAARIFA YA AJALI KAZINI AU MARADHI

i. Tarehe ya ajali kazini au maradhi .....
ii. Tarehe ya kupata ushauri wa mwanzo na Daktari kituoni .....iii.
Hali ya mwajiriwa wakati wa kutathminiwa .....
iv. Ugonjwa .....

D. TATHMINI YA DAKTARI

HALI YA SASA YA MWAJIRIWA - Weka (√) katika chumba kinachostahiki

i. Hali ya Mwajiriwa

Amepona kikamilifu na kurejea kazini na majukumu bila ya ulemavu wa kupoteza kiungo au kufanya kazi kiungo	Kwa mujibu wa karatasi ya hospitali ni siku ngapi mjeruhiwa / mgonjwa hakuhudhuria kazini

ii. Kwa kupoteza sehemu ya kiungo na kurejea kazini (Jaza Jadweli ya chini)

Amepona na kupata ulemavu wa kudumu wa kupoteza kiungo au kiungo kushindwa kufanyakazi.	Taja sehemu ya mwili iliyoathirika	Asilimia ya kupoteza kiungo husika au kutofanyakazi kiungo kwa mujibu wa kanuni (Jadweli la Tatu la Kanuni)

iii. Kwa kupoteza sehemu ya kiungo au maradhi na kushindwa kurejea kazini na bila ya kuhitaji msaidizi (jaza jadweli ya chini)

Kupatwa na ulemavu na kushindwa kabisa kurejea kazini	Taja sehemu ya mwili iliyoathirika iliyopelekea mfanyakazi kutoweza kurejea kazini.	Weka asilimia ya ulemavu pale mfanyakazi anaposhindwa kurejea tena kazini

iv. Ulemavu wa jumla unaosababisha mfanyakazi kubakia kitandani milele na kuhitaji msaidizi.

Taja kiungo kilichoathiriwa na kupelekea ulemavu wa jumla wa kudumu	Asilimia ya kutojiweza kunakohitaji msaidizi

v. Kifo kilichotokana na ajali kazini au maradhi yatokanayo na kazi yaliyopelekea kifo kwa mfanyakazi

Ainisha kiungo/viungo vilivyoathiriwa kutokana na ajali kazini au maradhi yatokanayo na kazi	Asilimia ya kifo kitokanacho na kazi

UTHIBITISHO

Mimi nathibitisha kuwa niliyoyasema hapo juu ni ya kweli kwa mujibu wa ufahamu wangu

Jina la Daktari .....Cheo .....

Namba ya usajili .....Simu ya mkononi .....

Barua pepe .....

Saini..... Tarehe .....

Muhuri wa Ofisi

JADWELI LA TATU

VIWANGO VYA ASILIMIA ZA ULEMAVU WA KUDUMU

[Chini ya kanuni ya 34(3)]

	MADHARA	ASILIMIA
1.	Kupoteza viungo viwili	100
2.	Kupoteza mikono yote miwili au vidole vyote pamoja na vidole gumba	100
3.	Kupoteza uoni wa macho yote mawili	100
4.	Kupooza mwili mzima	100
5.	Majeraha yanayopelekea mtu kubaki kitandani milele	100
6.	Majeraha yoyote mengine yanayosababisha ulemavu wa jumla wa kudumu	100
7.	Kupoteza jicho la pili kwa mwenye jicho moja	100
8.	Kupoteza mkono wa pili kwa mwenye mkono mmoja	100
9.	Kupoteza mguu wa pili kwa mwenye mguu mmoja	100
10.	Kuathirika Moyo	100
11.	Kupoteza mkono kuanzia begani	70
12.	Kupoteza mkono baina ya kisugudi na bega	68
13.	Kupoteza mkono katika kisugudi	67
14.	Kupoteza mkono baina ya kiganja na kisugudi	60/65
15.	Kupoteza mkono kuanzia kiganjani	60
16.	Kupoteza vidole vinne na gumba la mkono mmoja	60
17.	Kupoteza vidole vinne	35
18.	Kupoteza dole gumba (Vifupachanda vyote viwili)	35
19.	Kupoteza kifupachanda kimoja	
20.	Kupoteza kidole cha shahada	
21.	vifupa chanda vitatu	10
22.	vifupa chanda viwili	8
23.	Kifupachanda kimoja	4
24.	Kupoteza kidole cha kati	
25.	Vifupachanda vitatu	6
26.	Vifupachanda viwili	4
27.	Kifupachanda kimoja	2

28.	Kupoteza kidole cha pete	
29.	Vifupachanda vitatu	5
30.	Vifupachanda viwili	4
31.	Kifupachanda kimoja	2
32.	Kupoteza kidole kidogo	
33.	Vifupachanda vitatu	4
34.	Vifupachanda viwili	3
35.	Kifupachanda kimoja	2
36.	Kupoteza mifupa ya kiganja cha mkono	
37.	Wakwanza au wapili (zaidi)	35
38.	Watatu, nne au watano (zaidi)	50
39.	Kupoteza mguu gotini au juu zaidi	70
40.	Kupoteza mguu chini ya goti	40
41.	Kupoteza mguu	40
42.	Kupoteza vidole vya mguu vyote	15
43.	Dole gumba, vifupachanda vyote	5
44.	Dole gumba, kifupachanda kimoja	2
45.	Mbali na gumba, ikiwa zaidi ya kidole kimepotea - kila kimoja	2
46.	Kupoteza jicho	
47.	Jicho limetoka	30
48.	Jicho halioni	30
49.	Lenzi imetoka	30
50.	Uoni haupo isipokuwa mwangaza tu	30
51.	Uziwi	
52.	Masikio yote	50
53.	Sikio moja	25
54.	Kupoteza Figo	25
55.	Kupoteza uzazi (Infertility)	60
56.	Kupoteza ini(liver)	50
57.	Kupoteza meno	20 kwa kila meno sita.
58.	Mimba kuharibika (Abortion)	30
59.	Kuvunjika Mbavu (Ribs FRACTURE)	50
60.	Kuungua moto: inategemea asilimia ya kuungua. Ikiwa asilimia ya kuungua ni zaidi ya 60 asilimia ya kuumia ni 100.	100.
61.	Wengu (spleen)	25
62.	Bandama (pan crease)	50
63.	Kibofu cha mkojo	40
64.	Mapafu(lungs) (kila moja).	50
65.	Pelvic	50
66.	Kuchanika kwa uchango mpana au mdogo	40

67.	Ubongo (brain injury) inategemea severity) (mild, moderate or severe)	30,60, 90.
68.	Kukatika ulimi	60
69.	Kukatika mdomo (kila mmoja)	50
70.	Kukatika pua	40
71.	Kupoteza harufu	30

1. Kupoteza kabisa matumizi ya kiungo kutachukuliwa ni kupoteza kiungo. Kiwango cha asilimia ya kutojiweza kutokana na kuathirika kwa kiungo chochote kutahesabiwa kuanzia 25 hadi 100 ya kupoteza kwa kiungo cha mwili kutegemea kwamba uathirikaji huo umekaa vibaya au afadhali kidogo.

2. Kwa mtu anaetumia zaidi mkono wa kulia, jeraha analopata kwa mkono wa kushoto, na kwa mtu anaetumia zaidi mkono wa kushoto jeraha analopata kwa mkono wa kulia yatachukuliwa kuwa ni asilimia 90 ya viwango vilivyowekwa hapo juu.

3. Pale panapotokea kuwa sehemu mbili za mkono zimeathirika, basi kiwango cha athari hakitokuwa zaidi ya kile kilichowekwa kwa kupoteza mkono mzima.

4. Pale yanapokuwepo majeraha mawili au zaidi, jumla ya asilimia ya malipo inaweza kuongezwa, na pale majeraha yanapokuwa ni ya mkono, mpango ufuatao wa hesabu utafuatwa:

   (a) Endapo vidole viwili vimeathiriika, jumla ya asilimia ya malipo itaongezwa kwa asilimia 20 ya malipo hayo;

   (b) Endapo vidole vitatu vimeathirika, jumla ya asilimia ya malipo itaongezwa kwa asilimia 30 ya malipo hayo;

   (c) Endapo vidole vinne vimeathirika, jumla ya asilimia ya malipo itaongezwa kwa asilimia 40 ya malipo hayo.

5. Mfanyakazi mwenye jicho moja tu, anapoajiriwa akaacha kumueleza ukweli huo mwajiri wake, iwapo atapoteza jicho linaloona, atastahiki kupata fidia ya asilimia 30 tu ya ulemavu.

Kwa madhumuni ya Jadweli hili, mfanyakazi mwenye jicho moja maana yake ni yule mfanyakazi aliepoteza uoni wa jicho moja.

IMETIWA saini tarehe 20 Septemba, 2023.

.....

(DKT. SAADA MKUYA SALUM)

Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha na Mipango

ZANZIBAR.

LIMEPIGWA CHAPA NA WAKALA WA MPIGA CHAPA MKUU WA SERIKALI -ZANZIBAR